TOLEO NO.62

# Khilafah

(DHUL-QA'ADA 1446 HIJIRIA —MEI 2025 MILADIA) ( Bei Tsh 2,000/= - Ksh 100/=)

NDIO SULUHISHO

## KWANINI NDANI YA NCHI CHANGA KUNAKUA NA VURUGU KATIKA CHAGUZI?




Ni jambo maarufu katika nchi changa mara nyingi unapokaribia uchaguzi, siku ya uchaguzi na mara baada ya kumalizika, huwa siku za khofu kubwa vurugu, vitisho hadi mauaji badala ya kuwa ni siku za furaha na utulivu kwa kuwa wanademokrasia wenyewe hudai huo ni muda wa kupitisha mchakato wa kubadilishana uongozi.. Ripoti za kilimwengu zinakadiria kuwa vurugu hutokea kwa takriban 19% kiulimwengu na takriban 58% ya chaguzi za barani Afrika. Mwanzoni mwa miaka ya 1990 ilifikia 86% kwa Afrika

Baadhi ya mifano ya ghasia na vurugu za uchaguzi katika baadhi ya nchi za Afrika:

Tanzania tangu uchaguzi wa kwanza wa Rais wa vyama vingi uliofanyika mwaka 1995, kuibuka kwa ghasia kabla na baada ya uchaguzi ni jambo la mfululizo na lisilosita kila baada ya miaka mitano.

Vurugu mbaya na ya kusikitisha zaidi ilitokea katika uchaguzi wa mwaka 2000 ambapo zaidi ya wafuasi 40 wa

*Inaendelea uk ...2*

**Yaliyomo :**


- **Kila la Kheri Mahujaji watarajiwa - uk.3**
- **Uharamu Michanganyiko holela katika harusi —uk.4**
- **Sulhu Hudaibiya Inavyopotoshwa—uk.5**
- **Vita ya kibiashara baina ya China na Marekani —uk.7**
- **Malezi kwa Usahihi– uk. 8**

wa chama cha upinzani (CUF) visiwani Zanzibar waliuawa kwa kupigwa risasi, zaidi ya 600 kujeruhiwa na inakadiriwa 2,000 kukimbilia nchi jirani ya Kenya, wakati vyombo vya dola vilipofyatulia risasi umati wa watu walioandamana kupinga matokeo ya uchaguzi huo.

Mifano mingine ya vurugu za uchaguzi ni Disemba 2007 hadi Februari 2008 nchini Kenya ambapo zaidi ya watu 1,200 waliuawa na wengine 350,000 walikimbia makazi yao, mwaka wa 2010 katika uchaguzi wa Côte d'Ivoire takriban watu 3,000 waliuawa, Senegal mwaka 2012 ilipelekea vifo vya watu 15. Bila ya kusahau vurugu za mwezi Novemba mwaka jana nchini Msumbiji ambapo zaidi ya watu 50 wameuawa. Hii ni mifano michache sana katika matukio mengi.

Suala msingi sasa ni kuangazia sababu za vurugu hizo ambazo ni kama zifuatazo:

1.Nidhamu ya kisiasa ya kidemokrasia iliyochipuka katika mfumo wa kibepari unayachukulia 'maslahi' kuwa ndio msingi na kipimo chake katika mambo yake yote. Kwa hivyo, wanasiasa wote chini ya mfumo wa kidemokrasia iwe nchi changa zinazoigaiga mfumo huo, au nchi kubwa zilizojionesha kwamba ni vinara wa mfumo huo, uwepo wao ndani ya siasa ni kwa ajili ya kuyafikia maslahi binafsi. Kwa hivyo, wanasiasa huwa wako tayari kufanya lolote ili kuhifadhi maslahi yao. Zaidi ya hayo pia nidhamu ya kidemokrasia inashikilia fikra za Machieveli zinazohubiri msimamo usemao: '*njia yoyote ni halali ikiwa itafikisha kwenye lengo*'. Katika demokrasia ni halali kwao kutenda chochote hata kiwe na madhara kiasi gani ili kufikia wanakodhamiria.

Kwa maumbile hayo ya demokrasia, ni wazi nidhamu hiyo ni tete na bomu la kutega ambalo wakati wowote linaweza kuzaa ghasia, vurugu na ugomvi.

Inaweza kusemwa mbona vurugu hudhihirika zaidi katika nchi changa. Ni kweli, lakini haina maana kwamba katika nchi kubwa hakuna vurugu kama ambavyo tumeona karibuni katika uchaguzi wa Marekani. Isipokuwa katika nchi changa vurugu hudhihirika wazi zaidi, kwa kuwa kuna ukosefu wa taasisi thabiti kuwadhibiti watawala, kinyume na madola makubwa ya kibepari ambapo kwa kiasi fulani hujifichaficha kwa uwepo wa kiasi fulani wa utaasisi katika vyombo vyao unaotoa kiasi fulani cha udhibiti kwa wanasiasa na kuwafanya wayaendee maslahi yao kimahesabu katika vitendo vyao vya ufisadi nk.

Zaidi ya hayo nchi changa tofauti na nchi kubwa zenye mfumo, nchi changa hazikujengwa juu ya maslahi mapana ya kinchi. Jambo hili ni lenye kutarajiwa kwa kuwa ni nchi 'tawaliwa' ndio maana hazina sera thabiti za ndani na nje, wala hazikubeba mfumo, kwa mfumo huo ziwe na lengo la kujitawanya, kujijenga au kutangaza mfumo wao kimataifa. Bali kinachohirika kila mtawala huja na ajenda ya maslahi ya tumbo lake, familia na wapambe wake.

Hivyo, kwa mtawala wa aina hiyo kwake uchaguzi huwa jambo la kufa na kupona kuhifadhi maslahi yake hata ikiwa ni kwa gharama ya kumaliza wengine wote.

2. Katika nchi changa mara zote vyama vya siasa, viwe vilivyomo madarakani au vya upinzani, huwa kimsingi sio milki ya wananchi wala wanasiasa, bali huwa ni milki ya madola makubwa. Kwa leo vyama amma viko katika himaya au vinaungwa mkono na Marekani au Uingereza ambayo mara nyingi hujumuika na Jumuiya ya Ulaya. Katika hali kama hiyo, mabwana hawa wa dunia kila mmoja hutaka chama chake kishinde ili kidhamini maslahi yake. Kwa hivyo, chaguzi huwa za wananchi kwa jina tu, lakini kiudhati huwa ni ushindani mkali wa mabeberu kwa mgongo wa raia. Hali hii ni tofauti na chaguzi zao nchini kwao, ambapo vyama huwa vyao wenyewe.

3. Vyama vya siasa katika nchi changa hususan 'vilivyopigania 'uhuru wa bendera' ambavyo asili viliundwa na wakoloni na kupatiwa utawala baada ya uhuru wa bendera vimerithi dhana ya kikoloni, ya wao kuona wana 'hati miliki' ya kutawala nchi peke yao. Urathi huu wa kikoloni waliupata kwa kuwa vimetawala kwa muda mrefu katika mfumo wa chama kimoja na kujengwa nao na mabepari, kiasi cha watawala hao licha ya kujinadi kuwa ati walimfukuza mkoloni, lakini wako katika tabia ile ile ya mkoloni kuona wao wana haki zaidi kutawala kuliko wengine. Katika hali kama hiyo mfumo wa vyama vingi umekuja kuwaondoshea haki yao ya msingi ambayo wanahisi wa

***Inaendelea uk….6***

# KILA LA KHERI MAHUJAJI WATARAJIWA, LAKINI YAZINGATIENI NA HAYA

Tumeingia ndani ya mwezi wa Dhul-Qaadah ambao ni mwezi wa maandalizi ya mwisho wa safari ya ibada adhimu ya Hijja.

Waislamu wanaokusudia kufanya Hijja mwaka huu mashariki na magharibi wanakamilisha kwenda kutekeleza nguzo ya tano ya Uislamu ambayo ni wajibu kwa mwenye uwezo.

Wakati maandalizi kwa ajili ya safari ya kuitikia agizo hilo la Allah Taala yakipamba moto, mahujaji watarajiwa wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

Awali, mahujaji watarajiwa katika ibada yao huwa wanailenga misikiti mitakatifu. Yaani Masjid Haram wa Makka na pia kuuzuru Masjid Nabawi wa Madinatul Munawara. Basi mahujaji hawana budi wafahamu kwamba misikiti hiyo miwili haipo katika usimamizi mwa utawala wa Kiislamu, ambapo watawala madhalimu wafalme wa Saudia wananajisi misikiti hiyo kwa kunajisi ardhi yake ambayo ni kitovu cha Uislamu.

Aidha, mahujaji watarajiwa waelewe kuwa kando na misikiti hiyo miwili mitukufu pia Msikiti mtukufu wa tatu yaani Masjid Aqswa nao pia upo katika mikono ya mayahudi wanaendelea kuunajisi na kuondolea hadhi, heshima na utukufu wake.

Amma la pili la mahujaji



watarajiwa kulielewa, ni kuwa pamoja na kuwa ibada ya Hijja ni ibada tukufu ambayo hulenga misikiti mitukufu lakini kwa mujibu wa Mtume Saaw, damu ya Muislamu ni tukufu zaidi na ina thamani zaidi hata kuliko Masjid Haram yaani Kaaba.

Kwa mambo mawili hayo ya misikiti mitukufu kunajisiwa, na damu ya Muislamu kuwa tukufu kuliko misikiti hiyo, haina maana kwamba Waislamu wajizuilie kufanya ibada ya Hijja, bali ina maana kwamba licha ya kufanya ibada hiyo Waislamu waone dhima na jukumu kubwa kwenye mabega yetu la kuikomboa misikiti yetu mitukufu kutoka katika wasimamizi waovu na madhalimu wasiojali hadhi wala heshima ya misikiti hiyo na kulinda, kuhifadhi na kutetea damu ya Waislamu. Ambapo leo damu ya Muislamu ina thamani duni na inamwaga kila dakika na makafiri. mbele ya makafiri. Tunayashuhudia yanayoendelea Kashmiri, Burma, Turkistan bali hali ya kutisha zaidi na kuhuzunisha ni mauaji ya maangamizi ya halaiki ya Waislamu wa Gaza yanayotendwa na Israili kwa kuwezeshwa na Marekani na mataifa mengine ya magharibi kwa karibu mwaka na nusu sasa. Sio tu Waislamu wa Gaza wanauliwa kwa kwa mabomu na bunduki, bali wanauliwa kwa silaha ya njaa, kiu na kunyimwa huduma za kimatibabu kutokana na Israel na watawala vibaraka kuwazuilia kuingia ndani ya Gaza aina zote za misaada.

Wakati tukiwatakia mahujaji watarajiwa safari njema ya kwenda kuitikia mwito wa ibada wa nyumba tukufu. Vivyo hivyo tunawanasihi mahujaji licha ya kuitumia ibada hiyo kuwaombea dua Waislamu wa Gaza na wengine wanaodhulumiwa, bali kubwa zaidi wawe tayari kufanya kazi ya wajibu ya kurejesha tena dola ya Khilafah inayopaswa kuanzia ulimwengu wa Kiislamu, kwa kuwa ndio pekee yenye uwezo wa kulinda hadhi na utukufu wa misikiti mitakatifu na kulinda na kuhifadhi kiukweli damu, heshima na mali za Waislamu.

**Mhariri**

**01 Dhu al-Qi'dah 1446 H**

**29/04/2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

## Kuingia Bwana Harusi Katika Ukumbi na Wanawake

**Swali**

Je inafaa bwana harusi kukaa ubavuni mwa bi harusi wake (ukumbini) ili amvishe mapambo. Wakati inaeleweka kwamba wanawake wote wamejihifadhi na wengi wao maharimu, baada ya hapo yule bwana harusi aondoke?

**Jawabu:**

**“-**Hakika ya mchanganyiko wa wanaume na wanawake ni haramu na dalili zake zimejaa. Maisha ya Waislamu wakati wa Mtume (SAW) na masahaba baada yake yanazungumza jambo hilo. Na haifai mchanganyiko isipokuwa kwa haja ambayo sharia imeikubali na *nass* ya Kitabu cha Allah au Sunna ya Mjumbe wake ikapatikana kuhusu haja hiyo, mfano kuuza na kununua, kuunga ukoo... n.k.

Hakuna *nass* inayojuzisha mchanganyiko wa wanaume na wanawake katika kumbi za furaha (harusi). Lakini kinachopatikana (katika *nass*) katika wakati wa Mtume (SAW) na masahaba zake ni kwamba wanawake walikuwa wanakuwa pamoja na bi harusi, wao na yeye peke yao. Na wanaume peke yao. Kwa hiyo mchanganyiko katika kumbi ni haramu bila ya kutofautisha (*ghair mustathnaa*). Na kilichopatikana pia katika harusi ni kumpeleka mke kwenye nyumba ya mumewe hapo inafaa wampeleke wanaume na wanawake kwenye nyumba ya mumewe kisha wanabaguka wanaume kutokana na wanawake…

Kwa hivyo, kupatikana kumbi za furaha bila ya kutengana, yaani



katika ukumbi mmoja sio katika kumbi mbili, hilo ni haramu. Na ikiwa tupu ziko wazi kama ilivyoenea sana (siku hizi) katika hali kama hizi basi uharamu unakuwa mkubwa. **Na pia kukaa bwana harusi ubavuni mwa bi harusi wake ikawa amezungukwa (bwana harusi) na wanawake maharimu na wasiokuwa maharimu hilo ni haramu, na hasa wakiwa tupu zao ziko wazi, jambo ambalo mara nyingi wanawake huwa hivyo wakiwa wamemzunguka bi harusi siku hizi…**

Ama kauli ya kwamba jambo hili ndio limeshazoeleka na kuenea, kauli hiyo hailifanyi la haramu kuwa ni halali. Na ni kauli yenye kurejeshwa kwa mwenyewe (*marduudun ‘alaa swaahibih)* kwa vile inapingana na sharia. Bali kuna hadithi zinazowasifu wale wanaoishika vyema dini yao kuwa ni kama mwenye kushika kaa la moto kutokana na mitihani inayomfika Muislamu pindi akishika vyema Uislamu wake.

**قال رسول الله ﷺ: «يَأْتِي عَلَى النَّاسِ زَمَانٌ الصَّابِرُ فِيهِمْ عَلَى دِينِهِ كَالْقَابِضِ عَلَى الْجَمْرِ»...." انتهى.**

Mtume (SAW) amesema: ***“Watu zitawafikia zama, mwenye kusubiri katika dini yake ni kama mwenye kushika kaa la moto”***… Mwisho.

Kwa hiyo, bwana harusi kukaa pamoja na bi harusi wake katika ukumbi wa mchanganyiko wa wanaume na wanawake ni haramu. Na pia kukaa bwana harusi katika ukumbi wa wanawake pamoja na bi harusi wake na wanawake wamewazunguuka maharimu na wasio maharimu ni haramu. Na yote hayo yakiambatana na kuwa wazi tupu za wanawake na wamejipamba kuvutia, hilo litakuwa haramu juu ya haramu…

Ama ikiwa katika ukumbi kuna maharimu zake tu (bwana harusi), hapo inafaa kwake kuingia ukumbini na kukaa pamoja na bi harusi wake na pamoja na hao maharimu zake na amvishe mapambo kisha atoke. Baada ya hapo waingie wanawake wengine.

**Ufupisho:**

**1.** Haufai mchanganyiko wa wanaume na wanawake katika kumbi za furaha, sawa ikiwa tupu ziko wazi au zimesitiriwa. Na ikiwa tupu zenyekuharamishwa ziko wazi, basi uharamu unakuwa mkubwa.

**2.** Haifai bwana harusi kuingia katika ukumbi wa wanawake ili aketi na bi harusi wake muda wa kwamba wanawake ajnabi wapo hapo ukumbini, hata kama atawaeleza hao wanawake kabla hajaingia ili wajisitiri miili yao, na wasimkurubie bwana harusi, wamkurubie maharimu zake tu… muda wa kwamba wanawake wengine ajnabi katika ukumbi

**Inaendelea uk….8**

## SULHU HUDAIBIYA INAVYOPOTOSHWA MAANA NA MALENGO YAKE

Moja ya matukio makubwa na yenye mazingatio muhimu kwa Umma wa Kiislamu ni tukio la Mkataba wa Sul-hu Hudaibiya lilitokea ndani ya mwezi huu wa Dhulqaada mwaka wa 6 Hijria.

Tukio hili kwa bahati mbaya limedandiwa na baadhi ya watu wasiokuwa na nia njema na Uislamu na kulifanya kama kichaka cha kuhalalisha mikataba haramu na kukuza nguvu za maadui na kudhoofisha Umma wa Kiislamu.

Hivi ni baadhi ya vifungu vya Sulhu Hudaibiya :

الرجوع عن العمرة هذا العام

1. Mtume SAAW na Mswahaba wasifanye ibada ya Umra mwaka huo,(wa sulhu) warudi mwakani kufanya ibada hiyo

Kifungo hii huchukuliwa na baadhi ya watu kuachana na misimamo ya Kiislamu kwa madai Mtume SAAW alifanya hivyo.

Ifahamike ibada ya Umra sio wajibu ni Sunna, pia Mtume SAAW alikubali kuacha ibada ya Sunna akiwa ameshafanikiwa lengo lake, nalo ilikuwa kuzima uadui uliokuwa umepangwa baina ya Makuraishi na mayahudi wa Khaibar. Hivyo, kitendo tu cha Makuraishi kuingia mkataba wa aina yoyote na Mtume SAAW, maana yake mpango wao na mayahudi umevunjika. Na hili ndio lililokuwa lengo kuu la Mtume S.A.W




هدنة عشر سنوات

2. Muda wa Mkataba ni miaka kumi

Hii ni tofati na mikataba inayo fungwa na wakoloni na vibaraka wao katika ardhi za Waislamu, mikataba isiyo na ufafanuzi wa ukomo. Mfano mkataba wa Camp David, Oslo nk. haina ukomo.

Pia Kiislamu ili ufungwe mkataba basi lazima iwe kuna jambo jengine la muhimu na la wajibu linakwenda kufanywa. Kwahiyo, lengo la mkataba inakua ni kuzuiya hili kwa muda ili lifanyike lile .

من جاء من قريش إلى النبي مسلمًا يُرد إلى قريش
ومن جاء من المسلمين إلى قريش لا يُرد

3. Atakayetoroka au kuondoka kwa Makuraishi na kukimbilia kwa Mtume SAAW basi atarudishwa. lakini atakayetoroka kutoka kwa Mtume SAAW kwenda kwa Makuraishi mtu huyo hatorudishwa.

Kifungu hiki huvamiwa na mwenye nia ovu, kwamba Mtume SAAW alikubali unyonge mbele ya Makuraishi na kuwapa nguvu makafiri, basi hata sisi inajuzu.

Ndio, tunaona leo watawala wote wa Arabuni wanahalalisha kukitambua kijidola cha mayahudi (Israel), na masheikh wao ni suala la muda tu nao watatoa fatwaa za kuwatambua rasmi mayahudi

Lakini kwa kifungu hicho ukiangalia kwa makini utaona mshindi na aliye juu ni Mtume SAAW na Waislamu na wala sio Makuraishi.

Kwakuwa kifungu kinamlazimisha kafiri wa Makka lau atasilimu abakie Makka, lakini pia mkataba huo huo unamlinda asifanywe chochote na Makuraishi akiwa humo Makka. Hii maana yake Muislamu huyo atakuwa huru kutangaza dini na kusilimisha wengine. Bila ya kusahau kwamba awali ilikua marufuku kulingania Uislamu ndani ya Makka, bali kwa kifungu hiki sasa inakua huru

Amma kifungu hicho kuruhusu Muislamu akaritadi na akataka kurudi kwa Makuraishi Makka anaruhusiwa kwenda tu, kwani atakuwa hana faida katika jamii ya Kiislamu.

Hivyo, Mkataba wa Hudaibiya ulikuwa na faida kwa Waislamu na ushindi, na baadhi ya maswahaba kwa jicho la haraka haraka walitaka kuona kana kwamba ni kuwapa nguvu Makuraishi, lakini Mtume SAAW alikua na jicho kali na la mbali zaidi la kisiasa na kuona faida ipo kwa Umma wa Kiislamu

Na Allah SWT akathibitisha hilo muda mchache mara tu baada ya kufikiwa kwa mkataba huo kama ilivyoelezwa katika Surat Fat-hi.

Kwa ufupi, Mkataba wa Hudaibiya ulileta tija zifuatazo:

1. Ulitoa fursa adhimu kwa Waislamu kufanya da'awa ndani ya Makka

2. Uliwawezesha Waislamu kusambaa kwa mapana marefu maeneo mbali mbali ambayo

**Inaendelea Uk ….6**

## Sulhu Hudaibiya *kutoka uk .5*

mwanzo ilikua hatari kwa wao kuyafikia.

3. Waislamu kuwa huru kwenda kufanya ibada ya Hijja na Umra

4. Dola ya Kiislamu ilifanikiwa kupunguza wingi wa maadui waliokuwa wanapambana na Uislamu na kuwagawanya.

5. Dola ya Kiislamu kutambuliwa rasmi na Makuraishi, jambo ambalo kwa Makuraishi lilikuwa pigo kubwa sana la kisiasa.

6. Dola ya Kiislamu ya Madina kujikuza kimataifa dola kwamba ni dola ya amani, hekma na busara. Lakini sio tena dola ya maeneo finyu bali sasa inatambulika kimataifa kwa kuwalazimisha Makuraishi kuingia mikataba ya amani na dola hiyo.

Mkataba wa Hudaybia utabakia milele kuwa somo kubwa la kisiasa kwa Umma wa Kiislam, juu ya namna ya kupambana na maadui, kuvunja nguvu za mjumuiko wao na kumalizana nao mmoja mmoja.

## Matukio ya Dhul-Qa'adah

1.Kuanzishwa kwa chama cha kutetea wanyonge (Alfodhoul)

(Kabla ya Utume wa SAAW)

2.Ambush ya Saad bin Waqaas (kabla ya Vita vya Badr)

3. Kuzingirwa kwa Bani Qurayzah

4.Mkataba wa Hudaybia




## Vurugu – *kutoka uk.2*

na haki ya kuilinda kwa gharama yoyote. Hivyo, sio ajabu kusikia wakisema ushindi upatikane kwa namna yoyote.

4. Katika baadhi ya nchi kama Kenya kuna athari za urathi wa ukabila kwa kiasi kikubwa ulioshtadi katika siasa, uliolelewa na kukuzwa tangu zama za wakoloni. Walifanya hivyo kwa kulipatia kabila moja au makabila fulani nafasi zaidi katika utawala kuliko makabila mengine. Ni wazi nyakati za uchaguzi huwa sio tu muhula wa kubadilisha kiongozi mtawala bali huwa ni vita vya watu kutetea na kuhami jamii yao na kabila lao au makabila fulani.

5. Nchi kubwa za kibepari daima zimekua na uchu wa utajiri na rasilmali mbali mbali zilizomo katika nchi changa, na ndio maana wakazitawala kwa nguvu (ukoloni mkongwe) na hali ya kimataifa ilipobadilika ikabidi wabadilishe mbinu kwa kutoa'uhuru wa bendera', lakini wakiwacha nyuma vibaraka wa kudumu chini ya mfumo wa chama kimoja ili wadhamini na kulinda maslahi yao (ukoloni mambo leo). Na baada ya wananachi kuchoshwa na vibaraka hao kwa dhulma zao na ukandamizaji wao ,na kujiri mabadiliko fulani kiulimwengu, nchi za kibepari wakaja na ujanja na mbinu ya kuasisi au kurejesha vyama vingi katika nchi changa. Hivyo, vyama vingi vimeletwa kijanja na wakoloni kupozapoza kiudanganyifu joto la wananchi baada ya kubanwa na madikteta waliowekwa na wakoloni kulinda maslahi yao. Kamwe havikuletwa kuwa ukombozi au kuwaletea maendeleo wananachi, tofauti na namna wananachi wanavyobeba jambo hilo kuwa ni jambo la kufa na kupona.

Chaguzi katika nchi changa kwa mabepari ni aina tu ya 'danganya toto' kwa wananchi, bali mshindi wao tayari wanae katika mfuko, naye ni yule atakaedhamini na kulinda maslahi yao. Mawazo ya wingi wa kura wanayo wananchi lakini sio mabepari mabeberu.

Chaguzi za namna hii kimaumbile hutarajiwa kuzaa machungu, khofu na vurugu. Raia waliomchagua mgombea mshindi hutaka mgombea wao aashike hatamu, na mtawala aliyepora ushindi kwa baraka za madola ya kibepari na kuungwa mkono nao japo nyuma ya pazi hujizatiti kujilinda kwa hali yoyote.

Hali ya vurugu na ghasia katika uchaguzi ni jambo la kusikitisha na kuhuzunisha sana. Kwa sababu ni husuma ndani ya nyumba kwa maslahi ya mgeni (mkoloni). Kama vinavyotumika vinavyoitwa 'vita vya ugaidi' kudhuru raia kwa maslahi ya wakoloni, vivyo hivyo katika chaguzi wanasiasa hutumia nguvu kubwa kujeruhi, kutesa na kuuwa watu wao ili warudi madarakani,na upinzani hufanya jitihada washike hatamu. Pande zote mbili hawataki mamlaka kwa ajili ya wananchi wao, bali kwa maslahi mapana ya wakoloni, na wao wakipata kidogo cha kuramba ramba. Kwa bahati mbaya wananchi nao hutapatapa kutaka mabadiliko ya kisiasa kupitia chaguzi hizi ili waboreshe maisha yao, kitu ambacho ni ndoto. Chaguzi huwa hazileti mabadiliko ya kimsingi, kwa kuwa nchi hizi hazikubeba mfumo

*Inaendelea Uk….8*

## Matokeo ya Vita ya Ushuru baina ya China na Marekani

Kuanzia mwezi wa April, 2025 bidhaa kutoka nchini China zinazoingia Marekani zinakabiliwa na ushuru wa hadi 245% kutoka Marekani. China Kwa upande wake nayo imeweka mpaka ushuru wa 125% kwa bidhaa za Marekani zinazoingia nchini humo. Hali hii inasababisha wateja, biashara na masoko kutokua na uhakika, huku khofu kubwa ya mdororo wa kiuchumi duniani kote ikiongezeka, kwa sababu haya ni mataifa makuu mawili yenye uchumi mkubwa zaidi duniani kwa sasa.

Biashara kati ya China na Marekani imefikia hadi karibu $585bn (£429bn) mwaka 2024. Marekani iliagiza zaidi kutoka China ($440bn) kuliko China iliyoagizwa kutoka Marekani ($145bn). Kwahiyo nakisi ya kibiashara ya Marekani kwa China mwaka 2024 ni $295bn. Nakisi hii ni sawa na takribani 1% ya uchumi wa Marekani. Aina kubwa zaidi ya bidhaa inayouzwa nje kutoka Marekani kwenda China ilikuwa soya ambayo inatumika kulisha nguruwe takribani milioni 440 wa China. Marekani pia inapeleka dawa za binadamu na mafuta ya petroli nchini China. China kwa upande wake, inapeleka Marekani kiasi kikubwa cha vifaa vya elektroniki, kompyuta na midoli.




Aidha, Marekani inaingiza kutoka China simu za mkononi zinazochukua 9% ya jumla ya bidhaa zinazoagizwa nje.

Kwa mujibu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Marekani na China kwa pamoja zinachangia takribani 43% ya uchumi wa ulimwengu kwa mwaka 2025.

Ni wazi kuwa kujihusisha kwao na vita hii ya ushuru na biashara inaweza kupunguza kasi ya ukuaji wao wa kiuchumi au hata kuwasukuma kwenye mdororo wa uchumi, na hii itaathiri uchumi wa nchi nyingine za ulimwengu. Inaweza kupelekea ukuaji wa taratibu wa uchumi wa ulimwengu, mdororo wa uchumi na kuathiri uwekezaji wa kimataifa.

Kama Marekani na China hazitakuwa na makubaliano ya kupunguza ushuru, biashara kati ya nchi hizo mbili inatarajiwa kupungua kwa kasi, Hii itaifanya China kuja nmbadala wa kuchochea uchumi., ambapo Beijing itatanguliza viwanda na miundombinu ya kizamani, kama ilivyokuwa hapo awali vita hii ilipoanza mwaka 2018 badala ya matumizi na huduma, hii inaweza kusababisha ukuaji wa uzalishaji wa gesi chafu. Vita hii itaathiri mabadiliko ya nishati safi kwa China na ulimwengu .

China ambayo ni mzalishaji mkubwa zaidi wa gesi chafu duniani, akizalisha zaidi ya asilimia 30 ya uzalishaji wa kimataifa kuchochea uchumi wake ili kukabiliana na Marekani itakosa malengo iliyojiwekea juu ya upunguzaji wa hewa ya kaboni dioksidi. Na hili litaathiri ulimwengu mzima. Serikali ya Rais Xi Jinping imesema mara kwa mara kuwa iko wazi kwa mazungumzo, lakini ikaonya kwamba, ikiwa ni lazima, "itapambana hadi mwisho". Naye Rais Trump amesisitiza nia yake ya kupunguza ushuru wake kwa Uchina, lakini akasisitiza kuwa, hilo itategemea Beijing. Yote haya yanatuonesha jinsi gani mfumo wa ubepari na watawala wake walivyo binafsi wasiojali rmadhara mabaya kwa raia wao na kwa ulimwengu kutokana na vita hivi. Bali wao huangalia maslahi ya matajiri wachache na faida kubwa huku sehemu kubwa ya ulimwengu ikiangamia na kuteseka.

Vita hii ya kibiashara baina ya Marekani na Uchina ni dalili ya wazi kuwa ulimwengu unahitaji mfumo mbadala wa usimamizi wa haki na uadilifu kwa wanadamu, nao ni mfumo wa Uislamu chini ya dola yake ya Khilafah Rashidah.

Mfumo wa Uislamu uko kinyume na ubepari, umejengwa juu ya kipimo thabiti cha 'halali' na 'haramu', na sio faida na maslahi ya kibepari ambayo yamemuingiza mwanadamu katika nakama na mangamizi.

**USIKOSE KUSOMA JARIDA LAKO LA KHILAFAH KILA MWEZI**

## Vurugu – *kutoka uk.6*

wala haziko huru, bali ni 'nchi tawaliwa; zisizokuwa na maamuzi yoyote katika mambo yao ya msingi.

Kunahitajika mfumo mbadala utakaozikomboa nchi hizi kuwa huru na madola ya kibepari na pia kutoa dira thabiti itakayoleta ufanisi katika sekta zote za maisha.

……………..

## Maharusi uk ..4

wa furaha wapo wamekaa kwenye viti vyao wanashuhudia, yaani pale ukumbini. Basi hilo halifai.

**3.** Inafaa kuingia bwana harusi katika ukumbi wa furaha na kukaa pamoja na bi harusi wake, ukitengwa muda maalumu kwa ajili ya maharimu tu,

katika hali ambayo hapatakuwa na yeyote ukumbini wakati anapoingia na anapokaa pamoja na bi harusi wake isipokuwa maharimu zake. Kisha bwana harusi atoke, halafu tena waingie wanawake wengine baada ya kutoka yeye (bwana harusi).

**Sheikh Atta bin Khalil Abu Rashta**

**7 Muharam 1437** H **20 Oktoba 2015 M**

**Majibu ya maswala haya hujibiwa na Amiri wa Hizb ut Tahrir ( Allah Amuhifadhi) na hupatikana katika tovuti :**

***hizb-ut-tahrir..info***

## *Kurunzi ya Wanawake*

## *Usahihi wa Malezi ya Watoto*

Uislamu unatufundisha kwamba mtoto ni miongoni mwa neema na tunu kutoka kwa Allah Taala.

Kwa msingi huo suala la malezi mema ni wajibu kwa lengo la kuitunza neema hiyo tukufu, ambayo lau itakosa malezi mazuri itangamia.

Malezi mazuri ni sehemu mbili: Kwanza, huduma za kimada (vitu vitu) kama chakula, nguo, matibabu nk. Pili ni lazima kumpa mtoto katika maadili, yanayofinyanga haiba/shakhsia (personality) ya mtoto kwa mustakbali wake na kwa umma mzima.

Leo kilio juu ya watoto kukosa malezi mazuri kinasikika kila pembe. Sote huungana juu ya suala moja tu, kwamba watoto wetu wanakosa malezi mazuri kiasi cha kuwa watoto hao kuwa tishio la kugeuka 'bomu la kutega' dhidi yetu.

Tukiliangalia suala la malezi kwa upana tutaona kwamba mtoto hukabiliwa na malezi ya aina mbili. Malezi ya wazee wa mtoto katika familia na malezi ya jamii kwa ujumla wake.

Malezi haya yote aina mbili ni yenye kutegemeana daima, na tukitaka tupate watoto wenye malezi mazuri ya kweli, basi tusiyatenganishe malezi haya kwa kuwa huu ndio uhalisia ulivyo. Na tukiangalia kwa umakini zaidi tutaona kwamba, mtoto mara nyingi kama si zote, hujumuika zaidi na jamii hata kuliko na watu wake wa familia. Kwa mfano, mtoto huchukuwa muda mwingi kuwa shuleni, michezoni na pia madrassa, ukilinganisha na muda anaobakia na familia yake nyumbani. Kwa hivyo, malezi ya malezi ya jamii yanachukuwa sehemu kubwa na muhimu kwa mtoto hata kuliko malezi ya kifamilia. Japo kwamba kweli malezi ya familia nayo yana unyeti wa aina yake.

Ili kuweza kupatikana watoto wenye malezi mazuri kunategemea na jamii namna ilivyo, kwa maneno mengine, kutengenea kwa jamii kimaadili ndiko kwa kiasi kikubwa kutengenea mtoto katika jamii husika. Na kinyume chake, kuharibika jamii ndio pia sababu kwa kiasi kikubwa kuharibika kwa watoto wetu.

Maana ya 'jamii' Kiislamu, ni mjumuiko wa watu, fikra, mitazamo na vipimo vyao pamoja na nidhamu ya maisha inayoendesha maisha yao. Hii ina maana ikiwa watu wote ni Waislamu lakini wameathiriwa na fikra za kidemokrasia na nidhamu inayosimamia maisha yao si ya Kiislamu, hubakia watu hao kuwa Waislamu lakini jamii yao si jamii ya Kiislamu.

Leo Umma wa Kiislamu tumesibiwa na uovu mkubwa wa kuishi katika jamii isiyokuwa ya Kiislamu, jambo ambalo hutuathiri katika malezi ya watoto wetu na Uislamu wetu kwa jumla.

Utatuzi wa kudumu wa suala la malezi na mengineyo, inatubidi tujipinde Kuwalea watoto wetu tukiwa kama wazee kwa upande mmoja na kama Waislamu. Na kwa upande mwengine tuwemo katika mchakato wa kurejesha tena jamii ya Kiislamu. Jamii ambayo itajengwa juu ya vipimo vya Kiislamu pekee. Na jambo hilo litawezekana tu kwa kurejesha tena dola ya Kiislamu ya Khilafah.